

Ufisadi

Nchi yetu matatani, twazidi kupumbazwani,
Leo twazibwa machoni, kesho kweli peupeni,
Za vijana zi matatani, pesa hazijulikani,
Sisi tu vinywa nani, viongozi wetu zani.

Wengine wamezitia, pesa zetu mifukoni,
Msemo wao twasikia, vijana leo kazini,
Kesho tu uongozia, twajiuliza ni lini?
Kumbe kiwi kututia, sisi hatuna imani.

Yenyewe dhaifu pia, uchunguzi kila siku,
Leo kesho ongopea, ngapi zafanywa kikasuku,
Hatuna la kusifia, mengi kukashifu huku,
Nchi nini jivunia, kila kitu kama buku.

Kila siku sarakasi, sote mwelekeo giza,
Siasa chafu ni basi, twazurura hadi giza,
Hatujali 'lote sisi, muhimu twayapuuza,
Twaiba bila kiasi, tunataka kumaliza.

Kila mtu akilini wizi, tunapanga mikakati,
Usiku na mchana hizi, mipango tujifaiti,
Nafasi ni ndugu kazi, wengine kazi hapati,
Nchi hii tele simanzi, maskini maisha taiti.

Josphat Cheruiyot,
SEKU-Kitui.